

# **Ninafikiri au ninajua nilikuwa na COVID-19. Je, ni wakati gani ninaweza kuwa karibu na wengine?**

## **(sekunde 57)**

Ikiwa unadhani au unajua kwamba ulikuwa na COVID-19, unaweza kuwa karibu na watu wengine

- Baada ya siku 10 tangu dalili zilipojitokeza mara ya kwanza, **na**
- Baada ya saa 24 bila kuwa na joto kali wala kutumia dawa za kupunguza joto kali, **na**
- Baada ya dalili nyingine kuwa nafuu.

Ikiwa ulipatikana kuwa na COVID-19 na hukuwa **na dalili**, unaweza kuwakaribia watu wengine:

- Siku 10 baada ya kupimwa COVID-19

Ili kujifunza zaidi, tembelea [c-d-c dot g-o-v slash coronavirus](https://www.cdc.gov/coronavirus).